**KISWAHILI**

**Tarehe: 14/Juni/2024**

**Wakati: 8h30’-11h30’**

NESA NATIONAL EXAMINATION AND SCHOOL INSPECTION AUTHORITY

# MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU

| | |
|---|---|
| **KIWANGO:** | **Kidato cha Nne** |
| **MICHEPUO** | **LFK** |
| **MUDA:** | **Masaa matatu (3)** |
| **ALAMA:** | **...... /100** **CAMIS:** **...... /60** |

**MAELEKEZO**

- **Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.**
- **Mtihani huu unaundwa na sehemu kuu nne:**
    - **Ufahamu (alama 30),**
    - **Sarufi na Matumizi ya Lugha (alama30),**
    - **Fasihi (alama 25),**
    - **Utungaji (alama 15).**
- **Mtihani huu unaundwa na maswali 23.**
- **Jibu maswali yote kulingana na maelekezo yaliyotolewa.**
- **Tumia kalamu ya bluu au kalamu nyeusi**

**SEHEMU YA I: UFAHAMU NA MSAMIATI (Alama 30)**

**Soma hadithi ifuatayo, kisha ujibu maswali yaliyoulizwa juu yake.**

**Jongoo na Chura**

Jongoo na Chura walikuwa marafiki wakubwa sana. Kila wakati walitembeleana. Siku moja Chura alimwuliza rafiki yake Jongoo, "Rafiki yangu, huwa unafanya nini na ngozi yako? Mbona inang'aa sana? Tazama ngozi yangu, siyo laini. Ningependa iwe kama yako. Hebu nidokezee kidogo".

Jongoo alifurahi kuambiwa kwamba alikuwa na ngozi nyororo. Alianza kumpa rafiki yake ushauri kama ifuatavyo, "Rafiki yangu Chura, ngozi hii nyororo unayoiona ni kazi kubwa ambayo mke wangu amekuwa akifanya kwa muda wa miaka mingi. Kila asubuhi huweka kikaango motoni kisha hujaza mafuta na…"

Kabla hajamaliza, Chura alimkata kauli rafiki yake, "Basi, basi! Nimekwisha kuelewa. Huna haja ya kunielezea zaidi. Yote hayo nitayatenda na utaona nitakavyonawiri". Jongoo alijaribu kumshawishi amsikilize lakini Chura alisisitiza kwamba kwa utangulizi ule alikwisha kuelewa kila kitu. Marafiki wale waliachana. Jongoo alikwenda kwake na Chura pia alikwenda nyumbani kwake. Alipofika tu, Chura alimwita mke wake.

"Rwe! Rwe! Rwe!"

Naye mkewe aliitika, "Kororo! Rwe! Rwe!"

Chura alianza kumweleza mkewe, "Mke wangu, leo rafiki yangu amenieleza jinsi ya kuifanya ngozi yangu iwe nyororo na ya kung'ara kama yake. Sasa hivi nataka uweke chungo jikoni. Hakikisha jiko lina moto mkali sana." Mke alifanya kama alivyoelezwa. Chura aliendelea kutoa maagizo, "Nataka utie mafuta ya kukaangia mboga mengi sana na yakisha kuchemka nieleze mara moja".

Mkewe alitekeleza maagizo na mara akampa taarifa kwamba mafuta yalikwisha chemka. Chura aliingia jikoni akamwambia mkewe, "Sasa nitumbukize kwenye

mafuta kwani ninataka niibabue ngozi ya juu ili ibaki nyororo iliyopo chini yake". Mkewe alimjibu akiwa amepigwa na bumbuazi, "Mume wangu, mbona unaniambia nifanye kitu cha hatari? Kwani unataka kuniambia ukitumbukizwa katika mafuta yaliyochemka utapona! Haiwezikani hata kidogo. Balaa hilo lituepukie mbali!"

Chura alisisitiza kutumbukizwa katika mafuta na wakati huo alifanya hivyo kwa ukali.

"Mimi nimekuwa nikikuambia siku zote kwamba ngozi hii inanitia aibu. Leo nimepata njia ya kuiondoa nawe unapinga? Kaa chonjo tusikilizane. Si unaona jinsi ninavyokuaibisha kwa ngozi yangu yenye magamba! Ninatamani kuwa na ngozi nyororo mithili ya ile ya Jongoo. Nichemshie mafuta kisha unitumbukize katika kikaango.

Ewe mume wangu! Huoni kuwa nikikutumbukiza chunguni utaangamia? Haiwezekani. Katu katakata! Balaa hilo tuliepukie mbali. Alipokuwa akisema hayo, mzee chura alimkatiza na pupa akajitumbukiza katika kikaango na kuanza kulia "yoyoorwe! yoyoorwe!"

Mara moja mkewe akamuokoa kwa kumnyanyua toka katika kikaango na kumlaza mkekani. Halafu akawaita majirani kwa msaada, Mzee Chura akapelekwa mahututi hospitalini mara moja. Chura alipewa kitanda wiki nzima huku akijuta kuwa angalisikia ushauri wa mkewe msiba huo usingalimsibu.

Baada ya wiki kupita, Chura alirudi nyumbani. Alipoulizwa sababu ya kitendo cha kujitoma katika mafuta ya moto, alijieleza hivi: "Haya yote yalitokana na rafiki yangu Jongoo, nilipomuuliza sababu ya kung'aa kwa ngozi yake na kuwa nyororo alianza kuniambia alichofanyiwa na bibi yake kwamba anampaka mafuta yaliyochemshwa nikamkata kauli bila kuyamaliza maelezo yake. Nilipofika nyumbani nilimshurutisha mke wangu kunichemshia mafuta na kunitumbukiza ndani ya kikaango. Sikujua kuwa haya yote yangetokea."

Baada ya majirani kusikiliza haya yote, waliamua kumuita Jongoo ili ajieleze kwa nini alitoa ule ushauri wenye uovu kama ule. Jongoo alipofika alijitetea kwa maneno yafuatayo, "Ndugu zangu, mimi ninasikitika sana kwa yaliyomsibu rafiki yangu Chura. Yeye, aliniuliza kwa nini ngozi yangu inang'ara. Katika jitihada ya kumwelimisha kwamba mke wangu huchemsha mafuta halafu huyaweka pembeni yapoe kisha hunisugua nayo na baadaye huniweka juani ili ngozi ing'are zaidi, yeye Chura alinikata kauli hata kabla sijafika mbali kuelezea.

Alidai kwamba alishasoma mawazo yangu na hivyo alijua nilitaka kumaliza maelezo yangu vipi. Mara aliondoka akaja zake huku nyumbani." Wazee waliokuwepo pale waliamua kwamba Jongoo hakuwa na kosa, bali Chura alisababisha balaa hiyo mwenyewe kwa ujinga wake. Alijifanya kuelewa wakati ambapo hakuna alichoelezwa kikamilifu.

Huu ndio mwisho wa hadithi.

**Maswali ya ufahamu**

1) Taja wahusika wawili wanaozungumziwa katika hadithi. **(Alama 2)**

2) Taja uhusiano uliokuwa kati ya chura na jongoo. **(Alama 2)**

3) Chura alimuuliza nini Jongoo? **(Alama 2)**

4) Chura alikuwa na shida gani? **(Alama 2)**

5) Je, Chura alifaidika kwa mpango wake wa kubadilisha ngozi yake ili iwe laini? **(Alama 2)**

6) 6) Eleza jinsi Chura alivyopokea taarifa ambayo alipata kutoka kwa Jongoo. **(Alama 3)**

7) Mke wake Chura alipigwa na bumbuazi aliposikia maagizo ya mume wake. Kwa nini? **(Alama 3)**

**8)** Taja sababu ya Chura kusisitiza kutumbukizwa katika mafuta yaliyochemka. **(Alama 3)**

**9)** Hadithi hii imekufundisha nini? **(Alama 3)**

**10)** Fanya muhtasari wa hadithi hii katika aya moja isiyozidi maneno hamsini (50). **(Alama 5)**

**11)** Tunga sentensi kwa kutumia maneno yanayofuata kwa kuhakikisha kwamba umechunguza matumizi yake katika kifungu cha habari. **(Alama 3)**

**a)** Ngozi

**b)** Nyororo

**c)** kung'ara

## SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 30)

**12)** Tumia vitenzi vilivyo katika mabano kujaza nafasi tupu. (**Alama 4)**

**a)** Wangejua nia yangu katika kutetea haki za wanawake, ………………(kuchagua)

**b)** Ungeonana na daktari, ………………… (kutibu)

**c)** Vijana hawa wasingeendeleza uzembe, pesa zao ………. (kuongezeka)

**d)** ……………………umuhimu wa Kiswahili, wangekiteua kuwa lugha rasmi nchini mwao. (kujua)

**13)** Geuza sentensi zifuatazo katika hali yakinishi au hali kanushi. **(Alama 5)**

**a)** Msingetusalimia tusingewajibu.

**b)** Wangesoma kwa bidii wangeshinda mtihani huu.

**c)** Tusingefanya kazi kwa bidii tusingetajirika sisi sote.

**d)** Tusingalipata likizo, tusingalikwenda mjini.

**e)** Kioo kingalianguka, kingalivunjika.

**14)** Chagua kivumishi kinachofaa kwa kujaza nafasi tupu katika sentensi zifuatazo: **(Alama 5)**

**a)** Macho ……………. yanatazama majigambo ya watoto. (wachache, machache, vichache)

**b)** Katika kongamano la Kiswahili mambo ……….. ya kuendeleza lugha hiyo yaligusiwa. (vingi, pengi, mengi)

**c)** Makundi …………... ya wanafunzi yanawatembelea wagonjwa hospitalini. (vikadhaa, makadhaa, kadhaa)

**d)** Gari langu linateleza sana kwa sababu maji ………… yanajaa barabarani. (matele, watele, tele)

**e)** Magari ……… yalipatikana katika harusi yake. (chache, machache, wachache)

**15)** Watu wana maoni tofauti kuhusu asili ya kugha ya Kiswahili. Eleza maoni hayo kwa machache. **(Alama 5)**

**16)** Weka sentensi za hapo chini katika wingi au umoja. **(Alama 5)**

- **a)** Usijaribu kusema uongo wakati wa majadiliano.
- **b)** Usiwasihi watu kukubaliana na Mawazo amabayo hayalengi kudumisha amani.
- **c)** Ukipewa jaribio kuhusu mfano wa mdahalo, usinakili.
- **d)** Msidhani kwamba midahalo ni kama mijadala.
- **e)** Msisahau kutumia matamshi bora katika majadiliano.

**17)** **Orodhesha vizuri maneno yafuatayo ili yaunde sentensi zenye maana:** **(alama 6)**

**a)** walikuwa marafiki wetu sana watoto wakubwa

**b)** kimya kwamba kukaa nimekwambia sipendi.

**c)** makosa sababu kitu ya kufanya hakujibu Alipoulizwa.

## SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 25)

**18)** Taja aina tano za hadithi. **(Alama 5)**

**19)** Fasihi inahusianaje na utamaduni? **(Alama 6)**

**20)** Fasihi ni kioo na mwavuli wa jamii. Thibitisha kauli hii. **(Alama 5)**

**21)** Kamilisha methali zifuatazo: **(Alama 5)**

**a)** Leo ni leo asemaye ……………………..

**b)** Chelewa chelewa, ……………………….

**c)** Ndege aamukaye mapema, …………….

**d)** ……………… haina baraka.

**e)** ………………. ndio mwendo.

**22)** Taja vipengele vinne vya fani vinavyozingatiwa katika uchambuzi wa hadithi. **(Alama 4)**

**SEHEMU YA IV: UTUNGAJI (Alama 15)**

**23)** Chagua mada moja kati ya hizi zifuatazo kisha utunge insha yenye maneno kati ya 150 na 200.

**a)** Wadudu wanaotokana na uchafu na madhara yao.

**b)** Bila elimu hakuna maendeleo.

**Mwisho.**

**KISWAHILI**

**Tarehe: 14/Juni/2024**
**Wakati: 8h30'-11h30'**

# MWONGOZO WA KUKOSOA MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU

| | |
|---|---|
| **KIWANGO:** | **Kidato cha Nne** |
| **MICHEPUO** | **LFK** |
| **MUDA:** | **Saa tatu (3)** |
| **ALAMA:** | **...... /100** |
| **CAMIS:** | **...... /60** |

## MAELEKEZO

- **Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.**
- **Mtihani huu unaundwa na sehemu kuu nne: Ufahamu, Sarufi na Matumizi ya Lugha, Fasihi na Utungaji.**
- **Mtihani huu unaundwa na maswali 23.**
- **Jibu maswali yote kulingana na maelekezo yaliyotolewa.**
- **Tumia kalamu ya bluu au kalamu nyeusi**

**SEHEMU YA I: UFAHAMU NA MSAMIATI (Alama 30)**

**Soma kifungu cha habari kinachofuata, kisha jibu maswali yaliyoulizwa juu yake.**

**Jongoo na Chura**

Jongoo na Chura walikuwa marafiki wakubwa sana. Kila wakati walitembeleana. Siku moja Chura alimwuliza rafiki yake Jongoo, "Rafiki yangu, huwa unafanya nini na ngozi yako? Mbona inang'aa sana? Tazama ngozi yangu, siyo laini. Ningependa iwe kama yako. Hebu nidokezee kidogo".

Jongoo alifurahi kuambiwa kwamba alikuwa na ngozi nyororo. Alianza kumpa rafiki yake ushauri kama ifuatavyo, "Rafiki yangu Chura, ngozi hii nyororo unayoiona ni kazi kubwa ambayo mke wangu amekuwa akifanya kwa muda wa miaka mingi. Kila asubuhi huweka kikaango motoni kisha hujaza mafuta na…"

Kabla hajamaliza, Chura alimkata kauli rafiki yake, "Basi, basi! Nimekwisha kuelewa. Huna haja ya kunielezea zaidi. Yote hayo nitayatenda na utaona nitakavyonawiri". Jongoo alijaribu kumshawishi amsikilize lakini Chura alisisitiza kwamba kwa utangulizi ule alikwisha kuelewa kila kitu. Marafiki wale waliachana. Jongoo alikwenda kwake na Chura pia alikwenda nyumbani kwake. Alipofika tu, Chura alimwita mke wake.

"Rwe! Rwe! Rwe!"

Naye mkewe aliitika, "Kororo! Rwe! Rwe!"

Chura alianza kumweleza mkewe, "Mke wangu, leo rafiki yangu amenieleza jinsi ya kuifanya ngozi yangu iwe nyororo na ya kung'ara kama yake.Sasa hivi nataka uweke chungo jikoni. Hakikisha jiko lina moto mkali sana." Mke alifanya kama alivyoelezwa. Chura aliendelea kutoa maagizo, "Nataka utie mafuta ya kukaangia mboga mengi sana na yakisha kuchemka nieleze mara moja".

Mkewe alitekeleza maagizo na mara akampa taarifa kwamba mafuta yalikwisha chemka. Chura aliingia jikoni akamwambia mkewe, "Sasa nitumbukize kwenye

mafuta kwani ninataka niibabue ngozi ya juu ili ibaki nyororo iliyopo chini yake". Mkewe alimjibu akiwa amepigwa na bumbuazi, "Mume wangu, mbona unaniambia nifanye kitu cha hatari? Kwani unataka kuniambia ukitumbukizwa katika mafuta yaliyochemka utapona! Haiwezikani hata kidogo. Balaa hilo lituepukie mbali!"

Chura alisisitiza kutumbukizwa katika mafuta na wakati huo alifanya hivyo kwa ukali.

"Mimi nimekuwa nikikuambia siku zote kwamba ngozi hii inanitia aibu. Leo nimepata njia ya kuiondoa nawe unapinga? Kaa chonjo tusikilizane. Si unaona jinsi ninavyokuaibisha kwa ngozi yangu yenye magamba! Ninatamani kuwa na ngozi nyororo mithili ya ile ya Jongoo. Nichemshie mafuta kisha unitumbukize katika kikaango.

Ewe mume wangu! Huoni kuwa nikikutumbukiza chunguni utaangamia? Haiwezekani. Katu katakata! Balaa hilo tuliepukie mbali. Alipokuwa akisema hayo, mzee chura alimkatiza na pupa akajitumbukiza katika kikaango na kuanza kulia "yoyoorwe! yoyoorwe!"

Mara moja mkewe akamuokoa kwa kumnyanyua toka katika kikaango na kumlaza mkekani. Halafu akawaita majirani kwa msaada, Mzee Chura akapelekwa mahututi hospitalini mara moja. Chura alipewa kitanda wiki nzima huku akijuta kuwa angalisikia shauri la mkewe msiba huo usingalimsibu.

Baada ya wiki kupita, Chura alirudi nyumbani. Alipoulizwa sababu ya kitendo cha kujitoma katika mafuta ya moto, alijieleza hivi: " Haya yote yalitokana na rafiki yangu Jongoo, nilipomuuliza sababu ya kung'aa kwa ngozi yake na kuwa nyororo alianza kuniambia alichofanyiwa na bibi yake kwamba anampaka mafuta yaliyochemshwa nikamkata ulimi bila kuyamaliza maelezo yake. Nilipofika nyumbani nilimshurutisha mke wangu kunichemshia mafuta na kunitumbukiza ndani ya kikaango. Sikujua kuwa haya yote yangetokea."

Baada ya majirani kusikiliza haya yote, waliamua kumuita Jongoo ili ajieleze kwa nini alitoa ule ushauri wenye uovu kama ule. Jongoo alipofika alijitetea kwa maneno yafuatayo, “Ndugu zangu, mimi ninasikitika sana kwa yaliyomsibu rafiki yangu Chura. Yeye, aliniuliza kwa nini ngozi yangu inang’ara. Katika jitihada ya kumwelimisha kwamba mke wangu huchemsha mafuta halafu huyaweka pembeni yapoe kisha hunisugua nayo na baadaye huniweka juani ili ngozi ing’are zaidi, yeye Chura alinikata kauli hata kabla sijafika mbali kuelezea.

Alidai kwamba alishasoma mawazo yangu na hivyo alijua nilitaka kumaliza maelezo yangu vipi. Mara aliondoka akaja zake huku nyumbani.” Wazee waliokuwepo pale waliamua kwamba Jongoo hakuwa na kosa, bali Chura alisababisha balaa hiyo mwenyewe kwa ujinga wake. Alijifanya kuelewa wakati ambapo hakuna alichoelezwa kikamilifu.

Na huu ndio mwisho wa hadithi.

**SEHEMU YA I: UFAHAMU NA MSAMIATI (Alama 30)**

1) Taja wahusika wanaozungumziwa katika hadithi. **(Alama 2)**

**Jibu:**

**Jongoo, Chura pamoja na mke wake.**

2) Taja uhusiano uliokuwa kati ya chura na jongoo. **(Alama 2)**

**Jibu:**

**Chura na Jongoo walikuwa marafiki**

3) Chura alimuuliza nini Jongoo? **(Alama 2)**

**Jibu:**

**Chura alimuuliza Jongoo mbinu alizozitumia ili ngozi yake iwe laini.**

4) Chura alikuwa na shida gani? **(Alama 2)**

**Jibu**:

**Chura alikuwa na shida ya ngozi yake isiyo laini mfano wa ngozi ya Jongoo.**

5) Je, Chura alifaidika kwa mpango wake wa kubadilisha ngozi yake ili iwe laini? **(Alama 2)**

**Jibu**:

**Chura hakufaidika kamwe. Badala ya kubadili ngozi na kuwa laini ali, alifariki.**

6) Eleza jinsi Chura alivyopokea taarifa aliyopata kutoka kwa Jongoo. **(Alama 3)**

**Jibu:**

**Taarifa ambayo Chura alipata kutoka kwa Jongoo ilikuwa haijakamilika kwani aliambiwa aende akachemshe mafuta, akamtataza kuendelea kueleza kwa kuhisi kwamba yatakayofuata ameisha kuyaelewa kumbe aliyojieleza yalikuwa kinyume na maelezo ya rafiki yake Jongoo.**

7) Mke wake Chura alipigwa na bumbuazi aliposikia maagizo ya mume wake. Kwa nini? **(Alama 3)**

**Jibu**:

**Mke wake chura alipigwa na bumbuazi aliposikia mume wake anataka kutumbukizwa katika mafuta yenye moto, kwa sababu alijua agefanya hivo mume wake angefariki.**

8) Eleza sababu ya Chura kusisitiza kutumbukizwa katika mafuta yaliyochemka. **(Alama 3)**

**Jibu**:

**Chura alitaka aibabue ngozi yenye magamba na alitaka ile ya juu aiondoe abaki na ile laini ya ndani.**

9) Hadithi hii imekufundisha nini? **(Alama 3)**

**Jibu:**

**Hadithi hii inanifundisha somo la kutomkatiza mtu kauli yake kwa kuwa huenda nikapata habari isiyo kamili. Kwa kutopata habari kamiri ninaweza kupata hasara kama ilivyomfikia Chura.**

10) Fanya muhtasari wa hadithi hii katika aya moja isiyozidi maneno hamsini (50). **(Alama 4)**

**Jibu:**

**Msahihishaji atathmini muhtasari uliofanywa na mwanafunzi kwa kuzingatia taratibu za ufupisho.**

11) Tunga sentensi kwa kutumia maneno yanayofuata kwa kuhakikisha kwamba umechunguza matumizi yake katika kifungu cha habari. **(Alama 3)**

a) Ngozi

b) nyororo

c) kung'ara

**Jibu:**

**b) Ngozi: Ngozi ya kondoo ina sufu nyingi.**

**ch) nyororo: Muimbaji yule ana sauti nyororo.**

**d) Kung'ara: Viatu vya kiongozi wetu vinang'ara kila siku.**

**SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 30)**

12) Tumia vitenzi vilivyo katika mabano kujaza nafasi tupu. (**Alama 5)**

a) Wangejua nia yangu katika kutetea haki za wanawake, ………………(kuchagua)

b) Ungeonana na daktari, ………………… (kutibu)

c) Vijana hawa wasingeendeleza uzembe, pesa zao ………. (kuongezeka)

d) ……………………umuhimu wa Kiswahili, wangekiteua kuwa lugha rasmi nchini mwao. (kujua)

**Jibu:**

**a) Wangejua nia yangu katika kutetea haki za wanawake, wangenchagua.**

**b) Ungeonana na dakitari, angekutibu/ ungetibiwa.**

**c) Vijana hawa wasingeendeleza uzembe, pesa zao zingeongezeka.**

**d) Barabara zote zingekuwa za lami kila eneo nchini Rwanda, maendeleo yangesambaa nchini kote.**

**e)** ……………………umuhimu wa Kiswahili, wangekiteua kuwa lugha rasmi nchini mwao.

13) Geuza sentensi zifuatazo katika hali yakinishi au hali kanushi. **(Alama 5)**

a) Msingetusalimia tusingewajibu

b) Wangesoma kwa bidii wangeshinda mtihani huu.

ch) Tusingefanya kazi kwa bidii tusingetajirika sisi sote.

d) Tusingalipata likizo, tusingalikwenda mjini.

e) Kioo kingalianguka, kingalivunjika.

**Jibu:**

**a) Mngetusalimia tungewajibu.**

**b) Wasingesoma kwa bidii wasingeshinda mtihani huu.**

**c) Tungefanya kazi kwa bidii tungetajirika sisi sote.**

**d) Tungalipata likizo, tungalikwenda mjini.**

**e) Kioo kisingalianguka, kisingalivunjika.**

14) Chagua kivumishi kinachofaa kwa kujaza nafasi tupu katika sentensi zifuatazo. (**Alama 5)**

a) Macho ……………. yanatazama majigambo ya watoto. (wachache, machache, vichache)

b) Katika kongamano la Kiswahili mambo ………. ya kuendeleza lugha hiyo yaligusiwa. (vingi, pengi, mengi)

c) Makundi …………… ya wanafunzi yanawatembelea wagonjwa hospitalini. (vikadhaa, makadhaa, kadhaa)

d) Gari langu linateleza sana kwa sababu maji ………… yanajaa barabarani. (matele, watele, tele)
e) Magari ……… yalipatikana katika harusi yake. (chache, machache, wachache)

**Jibu:**

**a) Macho <u>machache</u> yanatazama majigambo ya watoto. (wachache, machache, vichache)**
**b) Katika kongamano la Kiswahili mambo <u>mengi</u> ya kuendeleza lugha hiyo yaligusiwa. (vingi, pengi, mengi)**

**ch) Makundi <u>kadhaa</u> ya wanafunzi yanawatembelea wagonjwa hospitalini. (vikadhaa, makadhaa, kadhaa)**

**d) Gari langu linateleza sana kwa sababu maji <u>tele</u> yanajaa barabarani. (matele, watele, tele)**
**e) Magari machache yalipatikana katika harusi yake. (chache, machache, wachache)**

15) Watu wana maoni tofauti kuhusu asili ya kugha ya Kiswahili. Eleza maoni hayo kwa machache. **(Alama 5)**
**Jibu:**
**Kuna maoni mbalimbali yaani mitazamo minne muhimu kuhusu asili ya Kiswahili: Mtazamo wa kwanza unatetea kuwa asili ya Kiswahili ni Kiarabu. Mtazamo wa pili hutetea Kiswahili kama lugha chotara, yaani mchanganyiko wa lugha za pwani na Kiarabu. Mtazamo wa tatu hutetea Kiswahili kuwa lugha ya kibantu, lakini mtazamo huu una mitazamo miwili ndani yake. Kwanza, lugha ya Kiswahili ilikuwepo toka zamani, kabla ya majilio ya wageni kwa baadhi ya watetezi. Kwa watetezi wengine,**

**lugha ya Kiswahili ni mchanganyiko wa lugha tofauti za Kibantu zilizotumiwa sehemu ya pwani.**

16) Weka sentensi za hapo chini katika wingi au umoja. **(Alama 5)**

a) Usijaribu kusema uongo wakati wa majadiliano.

b) Usiwasihi watu kukubaliana na Mawazo amabayo hayalengi kudumisha amani.

ch) Ukipewa jaribio kuhusu mfano wa mdahalo, usinakili.

d) Msidhani kwamba midahalo ni kama mijadala.

e) Msisahau kutumia matamshi bora katika majadiliano.

**Jibu:**

**a) Msijaribu kusema uongo wakati wa majadiliano.**

**b) Msiwasihi watu kukubaliana na Mawazo amabayo hayalengi kudumisha amani.**

**c) Mkipewa majaribio kuhusu mifano ya midahalo, msinakili.**

**d) Usidhani kwamba mdahalo ni kama mjadala.**

**e) Usisahau kutumia matamshi bora katika majadiliano.**

17) **Orodhesha vizuri maneno yafuatayo ili yaunde sentensi zenye maana: (alama 6)**

a) Watoto wetu walikuwa marafiki wakubwa sana
b) Nimekwambia kwamba sipendi kukaa kimya.
c) Alipoulizwa sababu ya kufanya makosa hakujibu kitu.

**SEHEMU YA III: FASIHI** (**Alama 25)**

18) Taja aina tano za hadithi. (**Alama 5)**

**Jibu:**

**Aina za hadithi:**

**a) Ngano: Aina ya hadithi ambayo wahusika wake ni watu tu.**

**b) Hurafa: Aina ya hadithi ambayo wahusika wake ni mchanganyiko wa watu, wanyama, miungu, mazimwi, na vitu vingine ambavyo hupewa uhai na kutenda kama watu.**

**c) Hekaya: Aina za hadithi ambayo wahusika wake ni mashujaa wa kitaifa.**

**d) Visakale/ Migani: Aina ya hadithi ambayo wahusika wake ni wanyama na vitu vingine ambavyo hupewa uhai na kutenda kama watu.**

**e) Soga: Hizi ni hadithi za kuchekesha na kukejeli**

19) Fasihi inahusianaje na utamaduni? **(Alama 6)**

**Jibu:**

**a) Fasihi husawiri na kuakisi jumla yote ya namna ya maisha ya watu. Kwa namna hii fasihi huakisi utamaduni wa jamii.**

**b) Fasihi hulinda jamii kwa kuhifadhi na kueleza vitendo vyake, vitendo vizuri vikihimizwa na kuchochewa, vitendo vibaya vikakatazwa.**

20) Fasihi ni kioo na mwavuli wa jamii. Thibitisha kauli hii. **(Alama 5)**

**Jibu:**

**Fasihi ni kioo na mwavuli wa jamii kwani fasihi hupata mambo yatendekayo katika jamii kama maovu na mema, na kuyawasilisha kwenye jamii hiyo kwa lugha ya kisanaa ambayo huelimisha wanajamii hivi wakiburudika na kustarehe. Papo hapo huwaonya watenda maovu kuacha maovu yao na kuwahimiza watenda mema kuendeleza matendo yao mazuri.**

21) Kamilisha methali zifuatazo: **(Alama 5)**

a) Leo ni leo asemaye ……………………..

b) Chelewa chelewa, ……………………….

ch) Ndege aamukaye mapema, …………….

d) ……………… haina baraka.

e) ………………. ndio mwendo.

**Jibu:**

**a) Leo ni leo asemaye kesho ni mwongo.**

**b) Chelewa chelewa, utamkuta mtoto si wako.**

**c) Ndege aamukaye mapema, hula wadudu watamu.**

**d) Haraka haraka haina baraka.**

**e) Polepole ndio mwendo.**

**22**) Tafa vipengele vinne vya fani vinavyozingatiwa katika uchambuzi wa hadithi. (**Alama 4)**

**Jibu:**

**a) Wahusika**

**b) Mtindo**

**ch) Muundo**

**d) Mandhari**

**e) Lugha**

**SEHEMU YA IV: UTUNGAJI (Alama 15)**

**23**) Chagua mada moja kati ya hizi zifuatazo kisha utunge insha yenye maneno 150.

a) Wadudu wanaotokana na uchafu na madhara yao.

**Jibu:**

**Baadhi ya hoja:**

**a) kutaja mifano ya wadudu watokanao na uchafu,**

**b) kueleza madhara ya kila mdudu,**

**ch) kutaja njia zinazoweza kutumiwa kuangamiza wadudu,**

**d) kuhimiza watu kuwa na usafi nguoni, mwilini na kadhalika**

b) Bila elimu hakuna maendeleo.

**Jibu:**

**Baadhi ya hoja:**

**a) Elimu hukuza uchumi wa nchi,**

**b) Elimu hutoa wananchi katika umaskini,**

**ch)Elimu huwasaidia wananchi kufahamu haki na majukumu yao katika kuendeleza nchi,**

**d) Elimu ni nyenzo bora za kupata maendeleo ya nchi,**

**e) Elimu hukuza uwezo wa wananchi wa kufikiri.**

**Mwongozo wa kukosoa insha (Alama 15)**

**FANI**

- Kichwa/ Mada: (**alama 2)**
- Urefu wa insha: (**alama 1)**
- Pembezo: (**alama 1)**
- Usafi: (**alama 1)**

**MAUDHUI**

- Utangulizi: (**alama 1)**
- Mwili: Maelezo ya hoja angalau tatu (**alama 7)**: Sarufi na matumizi ya lugha: **(alama 1)** (makosa mawili ni kutoa alama 0.5; makosa manne ni kutoa alama 1)
- Hitimisho: (**alama 2)**

**Mwisho.**